GREAT JOURNS

Journal of Kiswahili Vol. 1 No. 1, February 2022

# Matumizi Ya Uhalisiamazingaombwe Katika Uendelezaji MaudhuiKatika Riwaya Za Mhanga Nafsi Yangu Na Mashetani Wa Alepo

[1]Veronica Muhavi, [2]Dkt. Nilson Opande, [3]Dkt. Mahero Toboso.

*Chuo Kikuu Cha Kisii S.L.P 408 – 40200, Kisii*



***Ikisiri:*** *Makala haya yanadhamiria kuchanganua matukio ya uhalisiamazingaombwe katika riwaya za Mhanga Nafsi Yangu na Mashetani wa Alepo katika uendelezaji maudhui. Utafiti huu umejibana kwenye nadharia ya uhalisiajabu ambayo hujikita katika uajabu mwingi. Kupitia kwayo mtafiti alifanikiwa kupata maudhui kutoka kwa matukio katika riwaya teule kwani ndizo zilizo na matukio yaliyosheheni uajabu mwingi. Utafiti huu utawapa ari waandishi na wasomaji wa kazi za fasihi kuziandika na kusoma kazi zingine za uhalisiamazingaombwe. Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo uteuzi wa sampuli makusudi ndio uliotumiwa kupata vitafitiwa ambavyo ni Mhanga Nafsi Yangu na Mashetani wa Alepo. Sampuli hizi ndizo zilizotimiza upeo wa utafiti huu. Data nyingine ilipatikana kwa njia ya mahojiano na waandishi wa riwaya teule kama mbinu ya ukusanyaji data.Waandishi Said Ahmed Mohamed na Tom Olali wanaelezea matukio kwa njia ya ajabu. Wanatumia mbinu ya kifantasia, ndoto na hurafa ili kujenga msuko katika riwaya hizi wakiwa na lengo la kuelezea yale yanayofanyika katika mataifa mengi kwa njia fiche.Utafiti huu umetumia mtindo huu wa uhalisiamazingaombwe kupanua uwezo na uelewaji wa riwaya za kihalisiamazingaombwe ambazo huonekana tata na changamano kwa wasomaji wengi.*

## I. UTANGULIZI

Uendelezaji ni hali inayotumiwa na waandishi wa kazi ya fasihi kustawisha ujumbe ili uweze Kuifikia hadhira waliyonuia. Naye Senkoro (2006) anadai uhalisiamazingaombwe kuwa hali ambayo hukutanisha matukio ya uhalisia na mambo ya uchawi au yasiyo ya kawaida kwa hadhira. Anahodhi kuwepo kwa taswira nyingi katika kazi za uhalisiamazingaombwe ambapo matukio yaliyojaa fantasia hushuhudiwa. Wamitila (2008) anasema kuwa matukio mengi yanayopatikana katika kazi za uhalisiamazingaombwe huwa ya kinjozi yanapowekwa kwenye msingi wa ulimwengu halisi, matukio haya hukiuka au kuepuka kwa kiasi kikubwa kanuni za muhakati au mwigo wa maisha ya ulimwengu halisi. Matukio ambayo ni vigumu kuyaelezea katika msingi wa uhalisi na wa kawaida katika jamii. Kwa mfano ni vigumu kueleza jinsi Munene anavyofukuzwa na fuvu katika *Dharau ya Ini* au jinsi Kakulu anavyiweza kuongea, Kutania watu na kukimbia mara tu baada ya kuzaliwa katika *Mzingile*.

Matukio haya yanamfanya msomaji kuwa na taswira ya umazingaombwe akilini mwake. Matukio haya humjengea msomaji wa kazi za fasihi uwoga mwingi. Matukio haya hayawezi kupatikana katika hali halisi ya mwanadamu. Hata hivyo mtunzi hutumia umazingaombwe huu kufikisha maudhui muhimu katika jamii. Mbatia (1998) anataja uhalisiamazinaombwe kuwa istilahi inayotumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia yaani kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Anazidi kusema kuwa mazingaombwe hutokea pale ambapo matukio ya kihalisi huvamiwa na jambo ambalo ni la ajabu mno na ni vigumu kuaminika.

Cooper (1998) anadai kuwa uhalisiamazingaombwe ni mtindo katika fasihi unaotumia masimulizi ya kubuni na kifantasia yaliyojaa ufufuzi wa watu na matukio ya kimiujiza katika ulimwengu. Anaeleza kuwa uhalisiamazingaombwe hufumbata umoja na huwa na ukinzani dhidi ya historia na miujiza, ukoloni mamboleo dhidi ya mfumo wa kiuchumi, uhai dhidi ya kifo.

Akimuunga mkono Stretcher(1999) anasema mazingaombwe ni yale matendo ambayo hutokea pale ambapo matukio halisi huvamiwa na jambo ambalo ni la ajabu na ni vigumu kuaminika. Naye Green (2009) anasisitiza kuwa mtindo wa uhalisiamazingaombwe ulikuwa mtindo wa awali zaidi ambao ulitumika katika kaida za kiramsia ambapo masimulizi yaliyaweka sambamba matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida. Wafula na Njogu (2007) nao wanadai kuwa mtindo wa uhalisiamazingaombwe hukiuka sifa za uhalisia. Katika uhalisiamazingaombwe matukio yasiyoaminika husawiriwa. Mambo ya kiajabu huelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Matukio ya kushanagaza na kuogofya huwasilishwa na kuwa ya kawaida.

Khamis (2007) anasema kuwa uhalisiamazingaombwe hutumika sana katika kazi za fasihi ili kuyaelezea matatizo kwa msisistizo wa ndani kuliko nje. Aidha kazi za uhalisiamazingaombwe huwa na masimulizi ya kubuni ambayo huelezwa kwa njia ya mvunjiko wa matukio na huelezea uozo unaofanyika katika jamii kwa njia fiche. Naye Mkufya (1999) anasema kuwa huu ni mtindo ambao huchora maisha kiistari na kuyafananisha na maisha yaliyojaa sintofahamu za kiitikadi na siasa, uonevu, mabavu, uongo ugomvi na unafiki.

## II: MISINGI YA NADHARIA

Ili kutimiza azma ya Makala haya nadharia ya uhalisiajabu ndiyo iliyotumika katika kufafanua data zilizopatikana maktabani kuhusiana na riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Mashetani wa Alepo*. Nadharia ya uhalisiajabu iliasisiswa na mchoraji na mpigaji picha Franz Roh kutoka Ujerumani mwaka wa 1925. Roh aliziona picha zilizochorwa na kupakwa rangi kama zilizobeba uhalisia na uyakinifu wa maisha. Wakati huohuo picha hizo zilizobeba uajabu wa watu ndizo zilizoonyesha maisha ya watu katika

ulimwengu asilia. Akimuunga mkono Danow (1995) anasema kuwa nadharia ya uhalisiajabu hutumika kuelezea mambo ya kweli, ushetani, umizimu na mazingaombwe. Anasisitiza kuwa matukio ya kihalisiamazingaombwe hutokana na matendo ya kiajabu ya wahusika ambayo kutokea kwake huonekana kuwa ya kawaida.

S.A.Mohamed ni mwandishi aliyeandika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* akiwa amejikita katika mtindo wa uhalisiamazingaombwe katika kuendeleza maudhui anuwai. Ametumia matukio kwa njia ya ubunifu akiwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Ametumia matukio haya kuelekezea kidole cha shutuma kwa maovu yanayofanyika katika mataifa mengi ya Afrika. Hadithi nzima imejaa matukio ya kifantasia yanayowasilishwa kwa njia ya kimazingaombwe. Matukio ambayo humwacha msomaji katika hali ya uoga.

Wamitila (2008) anahoji kuwa matukio ni usababishi unaotawala maisha ya binadamu kwa kiasi kikubwa. Usababishi huu hukitwa katika matendo ya wahusika. Matukio katika kazi za fasihi hutekeleza wajibu muhimu katika kuendeleza maudhui. Waandishi wengi wa kazi za fasihi hubuni matukio kutoka kwa matendo ya wahusika na mazingira wanamopatikana. Matukio ndiyo hasa kitovu cha ujenzi wa maudhui anuwai katika kazi za fasihi.

*Mashetani wa Alepo* ni riwaya iliyoandikwa na Tom Olali. Riwaya hii imeosheheni utata katika matukio. Ni hadithi changamano ambayo ni vigumu kwa wasomaji kuelewa alilokusudia mwandishi. Mwandishi huyu amekiuka kaida za uandishi uliozoeleka wa uhalisia ambao hueleza matukio kwa uwazi. Jambo linalomwacha msomaji katika njia panda na kujihisi kuwa riwaya hiyo inakanganya na hivyo inapaswa kufafanuliwa zaidi kwa njia rahisi ili msomaji aweze kuelewa. Olali anatumia mtindo huu wa uhalisiamazingaombwe kwa njia ya kibunifu ili kuyajenga matukio yenye ufantasia. Matukio ambayo humfanya msomaji kuwa na uwoga na kuhisi kurekekebishwa akiwa na lengo la kuwatambua Mashetani katika jamii anamoishi.

Halikadhalika msomaji ataweza kufichua maovu yanayofanyika katika jamii anamoishi kama vile ufisadi, ukahaba, migomo ya wafanyakazi, ulanguzi wa dawa za kulevya, ukabila na vita. Matukio mengi katika riwaya hii yanatukia kwa njia tatanishi.

Waandishi Said Ahmed Mohamed na Tom Olali wameyaumba matukio ya uhalisiamazingaombwe wakiwa na lengo la kuendeleza maudhui.Riwaya hizi pia zinaweza kuitwa riwaya jirejelevu kutokana na sifa ya ujirejelevu katika muundo wake. Halikadhalika riwaya hizi zimeonyesha ubunifu mkubwa pale ambapo kuna maingiliano baina ya sauti ya kisimulizi na mhusika.

Hivyo basi uhalisiamazingaombwe ni mtindo katika fasihi ya Kiswahili ulio na dhima kuu katika uendelezaji maudhui. Mtindo huu huleta mvuto ambao husaidia katika uelewekaji wa maudhui. Matumizi ya uhalisiamazingaombwe katika riwaya hizi mbili umechangia katika kuchangamkiwa na kuongezeka kwa waandishi na wasomaji wa kazi hizi ambazo hapo awali zilionekana kuwa tata na zilizoonyesha mparaganyiko katika sarufi.

## 2.1 Mbinu za kukusanya Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ili kupata data kulingana na malengo yake na mihimili ya nadharia iliyochaguliwa.Sampuli makusudi ndiyo iliyoteuliwa kwa minajili ya kupata faafu. Sampuli hiyo ni riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Mashetani wa Alepo*. Riwaya hizi ziliteuliwa ili kutosheleza lengo la tatu ambalo lilihusu sababu za waandishi teule kutumia mtindo wa uhalisiamazingaombwe katika uandishi wao. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini na mahojiano na waandishi wa riwaya teule.

## 2.2 Matokeo ya utafiti

Katika makala haya kuna matukio mengi ya uhalisiamazingaombwe yanayojitokeza. Matukio haya yanatokea wakati kitu au mtu anapotenda matendo yanayovuka ukawaida. Matukio ni sehemu muhimu sana katika kazi ya fasihi hasa kazi zenye mtindo wa uhalisiamazingaombwe. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999) matukio mbalimbali katika kazi ya fasihi hutokana na matukio ya wahusika. Ni muhimu kuchunguza matukio kwa vile hakuna maudhui yanayoweza kupatikana pasipo na matukio ya wahusika. Kwa hivyo ili kujua kinachoendelea katika kazi yoyote ya fasihi lazima matukio yahusishwe na kuzingatiwa.

Olali (2010) anaeleza kuwa matukio ya uhalisiamazingaombwe katika kazi za fasihi huwa ya kifantasia au ya kiajabuajabu. Aidha kutokea kwake huonekana kuwa ya kawaida. Mara nyingi matukio haya huwa ya kutisha na ni vigumu kuyaelewa. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kuna matukio mengi ya uhalisiamazingaombwe yanayojitokeza.

**2.3 Mazingaombwe yanayohusisha mizuka**

Kuna tukio la kihalisiamazingaombwe linalotokea wakati Afida anapopanda ndege. Mzuka wa babake unamtokea akiwa kwenye vidato vya kuingia ndegeni na kuanza kuzungumza naye. Mzuka huu pia unaonekana ukiwa na matakwa ambayo Afida anapaswa kuyatekeleza. Tukio hili linapita ufahamu wetu kwani uhalisini ni vigumu sana mtu kupewa ushauri na mtu aliyekufa. Walio hai ndio hutoa nasaha. Tunaarifiwa kuwa babake Afida alifariki kitambo. Hatujaelezwa kama alifufuka. Kutokea kwake uwanjani mwa ndege ukiwa na matakwa yake kunaogofya. Tukio hili limeshinda ufahamu wetu. Tunaarifiwa kupitia kwa nukuu hii:

**Mfano (13)**

"Baadaye Afida alipokuwa akipanda chelezo cha ngazi, yaani *escalator*, baada ya kujigotoa na kupita uhamiaji, alishtukia akiwekewa mkono begani. Alipogeuka hakuona mtu. Hapohapo alijua kwamba huyo alikuwa babake. Labda naye alikuwa na maagizo naye akamweleza, "Nataka kusema yaleyale niliyokuwa nikikuambia kila siku kabla sijafa, kwamba mtu hujilinda mwenyewe." (uk15).

Tukio la Afida kuandamwa na mzuka wa babake popote aendapo ili kumwopoa na hatari za ulimwengu ni la uhalisiamazingaombwe. Tukio hili linaendeleza maudhui ya majukumu waliyo nayo wazazi ya kuwalinda wana wao.

**2.4 Mazingaombwe ya ndegeni**

Afida akiwa ndegeni kwenda Peponi, kuna tukio la uhalisiamazingaombwe linalotokea. Mzuka wa babake unamaliza mazungumzo naye na kupitia kwenye ufa wa dirisha la ndege. Tukio hili haliwezekani uhalisini, ni vigumu mtu kupita kwenye dirisha la ndege wakati ndege wakati ndege i angani kwa sababu kuna uwezekano wa mtu huyo kufa kutokana na anguko kubwa. Uhalisini ndege ndicho chombo pekee cha kusafiri kinachoweza kuelea hewani, Mtunzi anasema:

**Mfano (19)**

"Alipohitimisha maneno yake, baba mtu alirudi nyuma. Ilikuwa kama anaogopa kumpaka ujusi na ufu bintiye.Ghafla akapotea kwenye ufa wa kidirisha cha hili dege na Afida hakumwona tena kwa wakati huu."(uk20).

Mwandishi ametumia tukio la mzuka wa babake Afida kupitia kwenye ufa wa ndege kuendeleza maudhui ya mshikamano unaokuwepo katika jamii nyingi za Kiafrika. Waafrika wanaamini katika ushirikiano.

**2.5 matendo ya miujiza**

Mtunzi anaeleza tukio la kihalisiamazingaombwe lililofanywa na mzee Daudi ambaye ni babake Afida. Mzee huyu alikuwa na uwezo wa kuruka hewani na kwenda pahala popote anapopenda. Tukio hili haliwezekani katika hali ya kawaida kwani mtu hawezi kupaa angani kama ndege na kusafiri popote duniani. Na iwapo ataonekana akielea hewani bila shaka kuna nguvu za ajabu zinazomsukuma kutenda hivyo. Tunaarifiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano (21)**

"Aliweza hata kuruka hewani na kusafiri pahala popote alipopenda wakati wowote. Ni mara ngapi Afida wakati wa utoto wake alipolala na babake kitandani aligutuka usingizini na kumshtukia bwana huyo akizunguka kama pia na halafu akining'nia hewani kama tiyara isiyofungwa uzi."(uk 21)

Tukio la babake Afida kupaa angani na kuoneka akienda popote alipotaka ni la kimiujiza. Halikadhalika kule kuzunguka kama pia na kuning'inia hewani kama tiyara ni tukio lisiloweza kufanywa na mwanadamu yeyote. Ni vyombo tu vya kusafiria hewani na nyuni ambao huweza kuelea hewani. Tukio hili linaendeleza maudhui ya nguvu walizonazo waganga. Waganga wanaweza kufanya lolote wakitumia nguvu za ajabu ili waweze kuaminiwa. Vilevile tukio hili linaendeleza maudhui ya viongozi wabadhirifu ambao hutumia raslimali za wananchi kujistarehesha. Wao huweza kuzuru mataifa mbalimbali wakiwa na lengo la kujifurahisha huku wananchi wakiteseka katika umaskini.

**Mfano (40)**

"Kupitia lile dirisha wazi, lilopitisha mkondo wa upepo baridi, nilimshtukia babangu akitiririka chumbani kwa mzunguko wake wa pia…uleule mtiririko wa mazingaombwe ya bwana huyu tokea alipokuwa hai. Nilishangaa, maana inafika miaka miwili hajaja kunizuru hapa nilipo mbali na Motoni. Hakuja kwa hiki kizunguzungu cha pia. Mara nyingi alinitazama kwa mbali, akiupururia uhuru wangu…leo lakini kaja kinagaubaga, waziwazi, nyama na mifupa-kaja kamili kabisa." (uk 115).

Kuna matukio mengine ya uhalisiamazingaombwe yanayotendwa na babake Afida akiwa hai. Afida anadai kuwa babake alikuwa na uwezo wa kimiujiza ambapo aliweza kubadilisha changarawe kuwa njugu, karatasi kuwa noti ya shilingi za *King George* au *Queen Elizabeth*. Isitoshe kumgeuza mwanamume kuwa mwanamke. Haya ni matukio yanayoshinda ufahamu wetu. Kama tujuavyo changarawe ni mchanga na aliye na uwezo wa kubadilisha

chochote alichokiumba ni Mungu. Halikadhalika tukio la kubadili pesa haliwezekani uhalisini na kama lingewezekana kila mtu angekuwa tajiri. Hata hivyo mzee huyu huenda anatumia nguvu za uungu kutekeleza maajabu haya. Ushahidi mwingine unaoonyesha kuwa babake Afida hakuwa mtu wa kawaida ni wakati anapobadilisha mwanamume kuwa mwanamke. Tukio ambalo limewashinda hata wanasayansi ambao hutumia ujuzi na maarifa waliyonayoi uvumbuzi. Uwezo alionao babake Afida unatiliwa shaka kwa sababu unamithilishwa na ule wa Mungu. Tunaarifiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano (41)**
"Sikushangaa kwa kuja kwake hivyo kusema kweli.Babangu, kama unavyojua, alikuwa mtu wa miujiza alipokuwa hai isikwambii sasa akiwa mzuka kuna wakati niliamini miujiza yake bila ya kushuku. Sikudhani kwamba kile kilikuwa kiinimacho cha Babu pesa aliyebadilisha changarawe kuwa njugu, au karatasi kuwa noti ya shilingi za king George au Queen Elizabeth. Au inasemekana aliweza hata kumgeuza mtu mwanamume kuwa mwanamke-ingawa hilo mimi sikuliona."(uk115)

Wanauhalisiamazingaombwe hutumia mafumbo yaliyofichika ili kufanya kazi zao ziweze kueleweka na ziwe na fantasia nyingi. Kwa mujibu wa maandishi ya Roh (1925), anayedai kuwa kazi za uhalisiamazingaombwe hufumwa na matukio ya ajabuajabu. Matukio ya babake Afida kubadilisha changarawe kuwa njugu, karatasi kuwa pesa na halikadhalika mwamamume kuwa mwanamke ni ya ajabu. Matukio haya yanaendeleza maudhui mazito ambayo kwa kiasi kikubwa ni matendo ambayo hupatikana katika nchi za Afrika.Viongozi wengi hujikuta wakitenda maovu kama vile kujilimbikizia mali kwa njia isiyo halali.Wao hujihusisha katika biashara za magendo ambazo huwanufaisha wao wenyewe. Biashara hizo ni pamoja na ulanguzi wa dawa za kulevya, utengenezaji wa pesa bandia ambapo wao hujinufaisha huku mwananchi wa kawaida akiteseka. Viongozi hawa huwaalika hata wafanyabiashara kutoka mataifa ya Ulaya ili yaweze kufaidika na malighafi za Afrika. Mataifa haya hutoroka na malighafi ya Afrika yenye thamani na kutuacha sisi Waafrika tukihangaika jambo ambalo huzua migogoro kati ya mabwanyenye na maskini. Halikadhalika tukio la babake Afida kumgeuza mwanamume kuwa mwanamke ni tukio lisilowezekana katu kuaminika katika ulimwengu halisi. Mungu tu ndiye aliye na uwezo wa kuumba na kuumbua. Mwanadamu hajafikia kiwango hicho. Hata hivyo, Mwandishi ametumia tukio hili kuendeleza maudhui ya unyanyapaa walio nao viongozi wa Afrika. Wao hujiona kuwa bora na kuwadhulumu walio hoi.

Tendo jingine la uhalisiamazingaombwe linatendwa na mzuka wakati Afida yumo chumbani mwake. Anauona mzuka wa babake ukijitokeza ukiwa umevaa sanda. Tukio hili linamshangaza kwa sababu ni miaka mia moja tangu baba yake kuzikwa. Uhalisini mtu anapokufa huzikwa akiwa amevaa sanda. Tunatarajia kuwa baada ya miaka mia moja mfu awe ameoza na kinachobakia iwe ni mifupa tu. Hatutarajii sanda aliyovishwa iwepo kwa sababu ya kuoza kwake. Anajitokeza kwa njia ya mazingaombwe. Anaonekana akiwa anapepesa macho yake kwa ukali. Halikadhalika anaonekana akiwa na shungi kubwa la nywele kinyume na upara aliokuwa nao wakati wa mazishi. Jambo linalotushangaza mno ni namna anavyojitokeza. Tukio hili ni la uhalisiamazingaombwe kwani katika kazi za uhalisiamazingaombwe huwa kuna dhana nzima ya wakati. Matukio yanaacha kufuata uhalisi wa kiwakati.Miaka mia moja ya kifo na kuzikwa kwa babake Afida ni muda mrefu. Kile tunachokutana nacho hapa ni kioja ambacho hakiaminiki kamwe. Mtunzi anatuarifu kupitia dondoo hili:

**Mfano (43)**
"Alipotua mule chumbani,alitupa jicho hapa na pale kutazama hiki na kile kisha akalizungusha shungi akanitazama huku kauosha uso kwa bashasha na kicheko kitamu…Maruweruwe kidogo jinsi alivyo,kama mtu aliyerejea nyumbani baada ya miaka mia ya kupotea.Shungi kubwa la nywele limeota kichwani,kinyume na upara alikokwenda nao kaburini. Macho yake vilevile makali, maangavu yasiopepesa. Bado yana nguvu za kushawishi,lakini yamesimama wima kama twi! Kipaji kimeota sijida inayomeremeta kama lulu. Tofauti na alivyokuwa kabla hajafa…Mwili umepuuka ndani ya sanda iliyomvaa na kuraruka hapa na pale.Mchanganyiko wa harufu ulihinikiza mafuta mazuri yaliyomvaa baba kila alipokuwa akienda wakati wa uhai wake."(uk 116)

Tukio la babake Afida kumtokezea baada ya miaka mia ya kifo na pia akiwa na sanda aliyovishwa wakati wa mazishi ni tukio ambalo linamuacha msomaji kinywa wazi pasi na majibu. Vilevile mwandishi anatuarifu kuwa alikuwa anapepesa macho huku akiwa na shungi kubwa la nywele na kutoa harufu nzuri iliyohinikiza mafuta mazuri. Haya ni matukio ambayo hayawezi kuaminika kwa sababu inaonekana kuwa huyu babake Afida alikuwa anaendelea kuishi mle kaburini. Ile harufu nzuri iliyohinikiza ni tukio la kushanagaza kwa sababu alistahili kuwa ameoza. Uhalisini mtu anapokufa asipopelekwa makafani na mwili wake kutibiwa atatoa harufu mbaya. Kile kinachotushangaza ni kuwa alikuwa ameshazikwa na anapojitokeza ananukia harufu nzuri. Mtunzi ametumia matukio haya ya kihalisiamazingaombwe kuwasilisha maudhui mazito katika jamii. Tukio hili linaonyesha picha halisi ya hali ilivyo barani Afrika ambapo nchi nyingi zimejaa migogoro ya uongozi hasa baada ya kuondoka kwa ukoloni mkongwe,Waafrika walishangilia na kuamini kuwa sasa watajitawala wenyewe lakini mambo hayajaenda jinsi walivyotarajia,kumekuwepo na viongozi ambao wamejitokeza katika mataifa mengi ya Afrika na kurithi huo ukoloni mkongwe na kuuita ukoloni mamboleo.

kuna viongozi ambao hutumia nguvu na kuwanyanyasa raia wanyonge katika utawala wao.Viongozi hawa wameiga huo mtindo wa kiimla uliotumiwa na wakoloni katika kutawala na kuwadhalilisha Waafrika wenzao.

**2.6 Mazingaombwe ya Mwalimu Dawamu**

Kwa mujibu wa Zamora (2005), maandishi ya uhalisiamazingaombwe hubainika kati ya dunia mbili ya uhalisia na mazingaombwe. Dunia hizi mbili huwa zinawakilisha wafu na walio hai. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Mwandishi anaonyesha uhusiano kati ya mizuka na walio hai. Afida anapokuwa stani ya magari kuna tukio la kihalisiamazingaombwe linatokea. Anahisi baridi kali. Mara tu, fikira zinamjia jinsi Bi Marneti humuusia kuhusu baridi ya peponi. Ghafla anamwona mzee Dawamu aliyekuwa mwalimu wake wa fasihi. Dawamu alikuwa ni marehemu lakini alionekana akiwa amesimama mbele ya darasa akifunza. Ni vigumu tukio kama hili kufanyika uhalisini kwani mtu hawezi kufa, akazikwa baada ya miaka kumi aonekane akiwa darasani akifunza. Afida anamuona Dawamu kule Motoni akimsaidia kuchambua shairi la majina ya baridi Peponi.

Tukio la Mwalimu Dawamu kuonekana akiwa anafunza darasani ilhali alikufa kitambo haliwezekani katika ushabihikweli. Katika kazi za uhalisiamazingaombwe huwa kuna wahusika wafu ambao matendo yao huambatana na uhalisi fulani. Hii ni kwa mujibu wa Wamitila (2013). Mtunzi anasema hivi kupitia dondoo hili:

**Mfano (31)**

"Fikra hii pia ilimfufua mwalimu wangu wa fasihi, Mzee Dawamu kutoka kaburini huko alikoselelea kwa miaka. Sasa nilimwona kasimama mbele ya darasa letu kule Motoni, akitusaidia kulichambua shairi la majira ya baridi peponi. Akichambua huku akidengua fikra zote za ubwanyenye zinazosisitiza uzuri wa theluji na usafi wa hali ya hewa ya majira ya baridi. Au akionyesha uombolezaji wa washairi wa peponi kuhusu kukimbiwa na jua, ujoto, ujani, maua na ndege wazuri ingawa kwa kitambo Fulani." (uk 60)

Tukio la Afida kumwona mwalimu Dawamu akiwa darasani akichambua mashairi ya msimu wa baridi ni la mazingaombwe. Katika uhalisini tukio kama hili haliwezi kufanyika. Tukio la kumwona mtu aliyekufa kitambo akifanya shughuli alizokuwa akifanya akiwa hai haliwezekani uhalisini. Aidha tukio hili limetumiwa kuendeleza maudhui ya mazingira safi yapatikanayo barani Afrika. Pia tukio la mwalimu Dawamu kuonekana akifunza linaendeleza maudhui ya kihistoria. Watu wanaonywa dhidi ya kusahau utamaduni wao.

**2.7 Mazingaombwe yanayohusisha mizuka**

Kuna tukio jingine la kihalisiamazingaombwe linalofanyika wakati Afida anapokuwa katika fikira. Kizuu cha baba yake kinamjia kikiwa hai na kushiriki mazungumzo naye. Tukio hili ni la mazingaombwe kwa sababu kushiriki mazungumzo na mzuka si jambo la kawaida. Mizuka ni viumbe wa kufikirika tu ambao wanaaminika kuwa wafu. Uhalisini mtu anapokufa huwa amepoteza uhai na hawezi kuzungumza wala kutembea. Pia hafai kuonekana mbele ya watu. Lakini hapa tunakutana na mzuka wa babake Afida ukiwa hai wakati anapofikiri. Mzuka huu unamjia ili kutaka kumpa ushauri kutokana na hulka zake ambazo zimebadilika alipofika Peponi.

Tukio hili linazua hali ya kuogofya. Wamitila (2013) anasema kuwa katika kazi za uhalisiamazingaombwe kuna kukutana na wahusika mazimwi, wafu na mizuka. Hapa tunakukatana na mhusika mzuka wa baba Afida ambao unajitokeza wakati Afida yuko mawazoni na kushiriki naye mazungumzo. Tunaambiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano (32)**

"Mara nyingi kilinijia kizuu cha babangu. Kilinijia kizuu hai kunisusuika. Sikukwambia mimi Afida kwamba ungekuja wakati, babangu aliniambia, watoto wasingekuwa pamoja na wazazi wao? Sikukwambia mimi kwamba mwana asingemjali baba au mama? Dunia hii sisi wakati ule tuliita akheri dunia au heri zamani. Dunia inayoashiria kumalizika kwa dunia, ingawa nyinyi mnaita usasa na utandawazi."(uk 93).

Tukio hili ni la ajabu mno. Kukutana na mzuka ambao uko hai ni tendo la kuogofya. Isitoshe tendo la mzuka kufahamu yanayompitikia Afida kunashangaza kwa sababu babake Afida ni mhusika aliyefariki kitambo. Tukio la kumjia kama mzuka na kisha Afida amwone kama mwanadamu halisi ni tukio ambalo haliwezekani uhalisini. Maneno ambayo yanasemwa na mzuka wa babake Afida ni kweli. Tunakosa kujua kama mzuka uko hai na unashuhudia yanayotendeka kwani awali tumeambiwa kuwa babake Afida alikufa miaka mitano iliyopita. Mtunzi ametumia tukio hili la mzuka wa babake Afida kuzungumza naye kuendeleza maudhui ya kutowajibika kwa vijana hata baada ya wazazi kuwalea na kuwasomesha. Wazazi hawa huwa na matumaini makubwa na watoto wao. Watoto huwa kioo cha familia ambapo wazazi wamewekeza ndani wakijua kuwa watawafaa baada ya kufaulu. Hayo huwa hayafanyiki baada ya watoto hawa kufaulu. Riwayani tunamuona Afida akiwaahidi jamaa yake mambo mengi pindi tu afikapo ughaibuni. Lakini anapofika huko anawasahau wote na kuingilia maisha ya anasa. Vijana hawa huwaahidi wazazi wao usaidizi pindi tu watakapofanikiwa lakini mambo huwa hayaendi jinsi walivyoahidi kwani wanapobahatika kupata kazi na pesa, wao huwasahau wazazi wao na hata ahadi walizotoa. Mwandishi anawataka vijana watimize ahadi wanazotoa kwa wazazi kwani wazazi wamewalea na kuwaelimisha.

**III: MATUKIO YA UHALISIAMAZINGAOMBWE KATIKA MASHETANI *WA ALEPO***

**3.1 Mazingombwe ya Megido**

Kuna tukio la uhalisiamazingaombwe linalotokea Megido anapofungua macho yake na kuona maiti yake ikiwa imelala katikati ya kitanda chake. Hili ni tukio la kushangaza kwa sababu mtu hawezi kuwa katika hali mbili ila tu katika ulimwengu wa mazingaombwe. Riwayani Megido hajui kama yuko hai au maiti, kizuu au maiti hajui kama yeye ni kitu. Pia katika hii hali ya kuwa maiti na kuwa hai tunamuona Megido akijutia matendo maovu aliyoyafanya na kumuomba Mungu msamaha. Maovu haya ni pamoja na kuwaua watu, kuwabaka akina mama na watoto wao, kuchoma nyumba na makanisa. Tukio hili ni la kushangaza kwani mtu hawezi kuwa hai na ajione akiwa mfu. Uhalisini mtu anapokufa hana uwezo tena wa kuona tena hali yake. Pia mfu hawezi kujutia matendo aliyoyafanya akiwa hai kwa sababu hana uwezo tena wa kutazama. Kisa hiki cha mtu aliye hai kujiona akiwa mfu kitandani na kujutia matendo aliyoyafanya ni cha mazingaombwe. Tunaarifiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano (71)**

> Megido alifungua macho yake polepole. Maiti yake ilikuwa imelala katikati ya kitanda chake kikubwa. Megido hajui kama yuko hai ama mfu. Hajui kama yanayotokea ni ndoto ama ni ya kweli. Yeye ni kizuu? Yeye ni maiti? Yeye ni kitu? Mimi sijui. Walikuwa vizuu kupitia njia gani? Nani? Ninachokijua ni kuwa tuliwatendea visivyo." (uk 1-2)

Mwandishi ametumia tukio hili kuonyesha jinsi wanaoshiriki mapigano ya kimbari hupoteza matumaini ya kuishi baada ya kugundua kuwa waliyoyatenda hayakufaa.

Kwa mfano kuna wimbo unaochezwa akilini mwa Megido kwa sauti kubwa. Wimbo huu unamkumbusha Megido maasi aliyoyafanya. Jambo linalomsababishia kuumwa na kichwa kwa sababu ya sauti hiyo ya juu. Yeye Megido hali wala kunywa. Yeye ni maiti atembeaye. Tukio hili ni la ajabu kwani uhalisini ni vigumu wimbo kucheza akilini mwa mtu kwa sauti kubwa inayosikika. Akilini, mtu huweza kukumbuka aliyoyafanya bali sio kwa sauti kubwa. Pia mtu anapokufa hawezi tena kutembea. Mtunzi anatuarifu kupitia dondoo hili:

**Mfano(72)**

> "Maneno ya wimbo huo yanacheza akilini mwangu kwa sauti kubwa. Ninaumwa na kichwa kwa sababu ya sauti hiyo ya juu. Silali, sili, sinywi. Mimi ni mfu atembeaye. Au mimi ni kivuli tu. Mimi ni kivuli changu. Kweli mimi ni kivulichangu. Na kivuli kina uhai?...Dawa nataka. Dawa ya kunipa uhai. Mimi ni mfu hapa. Lakini sijapoteza matumaini ewe *Obong`o Nyakalaga*. Ninajua kuwa ili kuepuka kwenda Gehenna, ni sharti nibadilishe nyendo zangu…Jameni maneno katika wimbo 'walijuta' yananitia kiwewe. Ni kweli nimeshiriki wimbo wa jinamizi kwangu…Mungu wangu picha za nyumba nilizozichoma zingali zinanijia. Ninahisi moto wa gehenna. Picha za wale ambao niliwakatakata zingali akilini mwangu." (uk 6-7).

Tukio hili la wimbo kucheza akilini mwa Megido kwa sauti kubwa na kujiona akiwa maiti anayetembea linaendeleza maudhui ya majuto baada ya mauaji. Mwandishi anaonyesha jinsi vijana hutumiwa na wanasiasa kutekeleza mauaji ya kimbari kwa misingi ya kikabila huku wanasiasa wakistarehe. Baada ya mauaji ya kimbari, vijana walioshiriki mauaji hayo hukamatwa na kisha wakajutia yale waliyoyatenda huku wanasiasa waliochochea mapigano hayo wakiachwa huru. Pia mwandishi anatujulisha maovu ambayo yanatendeka katika mataifa mengi yakiwemo ubakaji, mauaji ya kimbari, uchomaji wa makanisa kutokana na uchochezi wa wanasiasa.

**3.2 Mazingaombwe ya akilini**

Tukio jingine la kiuhalisiamazingaombwe linafanyika akilini mwa Megido. Kuna matukio machafu yanayofanyika akilini mwake mnamo mwaka wa 3020. Akishirikiana na wenzake, wanapanga jinsi watakavyowaangamiza Wamaya. Sauti yake inayofananishwa na ya bundi inasikika ikiwaamuru wenzake kwenda kushiriki mapigano.

Tukio hili ni la uhalisiamazingaombwe. Mapigano hayawezi kufanyika akilini mwa mtu. Mapigano yanaweza tu kutokea katika nchi ama uwanjani. Sauti anayoitoa Megido inayomithilishwa na ya bundi ni ya kogofya. Uhalisini sauti ya mwanadamu haiwezi kuwa kama ya bundi kwa sababu bundi ni ndege aliye na sauti tofauti sana na ile ya mwanadamu. Katika uhalisi bundi ni ndege ambaye kutokea kwake huwa kunaashiria habari mbaya. Sauti anayoitoa Megido inaendeleza maudhui ya uchochezi kwa vijana na kuwataka kushiriki mapigano dhidi ya Wamaya. Mtunzi anatuarifu kupitia dondoo hili:

**Mfano (73)**

> "Kichwani mwa Megido kulitokea machafu mwaka wa 3020. Wamaya sharti wang`olewe ni mahawinde! Ni mahabithi! Ni mahayawani! Megido alisema kwa sauti ya ukali na kupasua huku

> akibigija Kamba aliyokuwa amebeba-kamba ya kufanya kazi. Sauti ya Megido ilikuwa na toni mbaya na iliogofya. Sauti ya bundi na yenye sumu. Macho makali ya hajivale yaliwatazama wenzake. Wamaya watatoka, Wamaya wataisha." (uk10-11).

Matukio yanayofanyika akilini mwa Megido kuhusiana na machafuko ya mwaka wa 3020 yanaendeleza mapigano ya kikabila yanayoshuhudiwa katika mataifa mengi ya ulimwengu. Mapigano haya mara nyingi huchochewa na viongozi wa kisiasa ambao huwatumia vijana kwa kuwapa kasumba ya chuki. Kasumba hii huwafanya vijana hao kushiriki vita vya kikabila na kusababisha ghasia na michafuko katika taifa.

### 3.3 Mazingaombwe ya ndoto

Megido anapokuwa kwenye maongezi na wenzake kuhusu uchaguzi na wizi wa kura, kuna njozi anayoishuhudia akiwa ameketi. Anamwona swila mkubwa akitoka kichakani. Kalausi anapomwambia kuwa hiyo ni ishara ya wao kutoendelea na safari Megido anakataa katakata na kudai kuwa walishapokea malipo kwa kila nyumba watakayoichoma na kanisa watakayoichoma. Watu wote walio karibu na Megido akiwemo Ribit wanajificha nyuma ya Megido kwani waliamini kuwa yeye ndiye aliyekuwa na dawa ya kumuua yule swila. Wanapigana na swila hadi kiwango cha kumuua. Nyoka yule anafariki kutokana na juhudi za Kalausi, Megido na Champion. Baadaye Megido anazinduka kutoka usingizini na kutaka kujua kama Wanyakwelekere wapo. Wote wanaitikia na kusema wapo. Anapotaka kujua iwapo walitishwa na swila, wote wanagutuka kwa kuulizwa swali hili kwa vile hawakushiriki mapigano yoyote. Megido anahisi maumivu na moyo wake unaenda kasi baada ya kugundua kuwa ilikuwa njozi ya kutisha. Hajui kama njozi ile ilikuwa na maana fiche au uhai. Mwandishi anasema kupitia dondoo hili:

**Mfano (75)**

> "Mbona sauti zenu hafifu jinsi hiyo. Mmechoka? Mmetishwa na swila? Kwa pamoja walimuuliza. Hawakufahamu. Hawakujua chanzo cha kuulizwa kama wametishwa na swila. Hadithi ya swila inatoka wapi? Hawakuwa wameshambuliwa na swila yeyote. Hakukuwa na joka lolote. Kicheko-fikira za Megido tu. Njozi ile ya kutisha alijua ilikuwa na maana. Maana fiche. Aliona soni kuuliza wenzake maana ya njozi hiyo.Njozi ina uhai." (uk 23-25).

Ni vigumu kwa tukio kama hili kutokea uhalisini hasa ikizingatiwa kuwa mtu anaenda kushiriki mauaji halafu akiwa njiani anaota akitembea kuhusu mapigano na swila. Anapozinduka anakuta hakukuwa na mapigano yoyote.

Tukio la Megido kuota akitembea na kuhusika katika mapigano na swila linaendeleza maudhui ya kushindwa. Aidha mtunzi ametumia tukio hili la ndoto ya mapigano kuonyesha umuhimu wa utangamano kati ya makabila yanayoishi katika bara la Afrika. Nyakati za uchaguzi raia wasikubali kugawanywa na wanasiasa ambao huwatumia vijana kuzusha ghasia.

Tukio jingine la uhalisiamazingaombwe linatokea wakati Ulrich Fusako anapoota akiwa anatembea. Anawaona wanyama wawili ambao ni Naningwanzula na Mjombakaka. Wanyama hawa japo ni wa spishi moja wanaonekana wakicheza mchezo wa bao lakini mjombakaka anavuruga mchezo kwa kuhamisha kete kutoka kwenye shimo hivyo kumnyima naningwanzula ushindi. Jambo linalozua mapigano makali kati ya wanyama hao wawili. Mara anatokea chura mbilikimo wa kidimbwi. Chura ambaye ni mdogo sana anayetumia kifuko chake kutoa sauti inayowapatanisha Naningwanzula na Mjombakaka na wanaacha kupigana. Ulrich Fusako kwa mara ya kwanza anawaona wanyama wakitabasamu. Kitendo hiki kinatendeka ndotoni akiwa anatembea.

Tukio la Ulrich Fusako kuota huku akitembea kuelekea kwa Wamaya kuenda kushiriki mapigano ni tukio la ajabu sana. Yale anayoyaona ndotoni kuhusu wanyama wa nanimgwanzula na mjombakaka yanalandana mapigano amabayo anataka kujihusisha nayo: mapigano kati ya Wamaya na Wanyakwelekere ambayo ni makabila yanayopatikana katika taifa la Alepo. Tunaarifiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano(77)**

> "Ulrich Fusako kwa mara ya kwanza aliwaona wanyama wakitabasamu. Namna gani? Alijiuliza. Alisubiri kwa hamu kushuhudia mapigano kati ya wanyama hao lakini hayo hayakufanyika. Ilikuwa vigumu kujua kama hii ilikuwa ni ndoto ama halisi iliyotokea. Kwa upande mwingine, Ulrich Fusako alikuwa katika ndoto nzito, ndoto ya kweli hasa-ndoto ya mjombakaka na aningwanzula wakikorofishana kwa ajili ya mchezo wa bao na mwamuzi chura mbilikimo wa kidimbwi-mhusika anayezima mauaji. Ndoto hii ilitokea akiwa anatembea. Ndoto ya kufanyika mtu anapolala…Na hii ilikuwa inafanyika akiwa anatembea na wenzake." (uk60).

Tukio la Ulrich Fusako kuota akitembea na kisha awaone wanyama Naningwanzula na Mjombakaka wakipigana

kwa Sababu ya kukosekana kwa haki wakati wa mchezo wa bao, kunaendeleza maudhui ya mapigano. Mapigano haya yameshuhudiwa katika mataifa mengi kutokana na wizi wa kura. Mapigano ambayo huhusisha makabila ambayo huishi katika taifa moja. Halikadhalika kitendo cha chura mbilikimo cha kuchukua kifuko chake na kutoa sauti inayowafanya Naningwanzula na Mjombakaka kupatana kunafanikisha maudhui ya mapatano ambayo hufanywa kati ya makabila mawili yanayozozana kisiasa katika taifa na wapatanishi.

**3.4 Mazingaombwe ya sauti**

Kuna sauti inayosikika ikimwita na kumkataza Kalausi dhidi ya kwenda kupigana na jamii ya Wamaya. Yule anayeita haonekani wala sauti yenyewe haijulikani ni ya nani. Tukio hili ni la uhalisiamazingaombwe. Uhalisini mtu huitwa na mwenzake. Hii sauti tunayokutana nayo katika riwaya hii inaibua hali ya kutisha. Mtunzi anaeleza kupitia dondoo hili:

**Mfano (78)**

> "Simama, wewe usiende. Mbona umeenda? Mbona, unaenda kuwaua ndugu zako wa Alepo? Kalausi alisimama. Tena ile sauti kwa nguvu zaidi. Simama wewe usiende kuwaua ndugu zako wa Alepo? Mara nyingine maneno yale yale kwa nguvu maradufu. "Simama wewe usiende. Mbona unaenda? Kuwaua ndugu zako? ( uk 26).

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kazi za uhalisiamazingaaombwe huwa na kukumbana na vitu visivyokuwa na uhai lakini vilivyopewa stadi na sifa za binadamu lakini binadamu mwenyewe haonekani. Ndiposa data hii inaendeleza maudhui ya onyo. Katika mataifa mengi ya uliwengu kunapotokea mauji ya kikabila huwa kuna shutuma kali zitokazo kutoka mataifa mengine na kuwaonya dhidi ya kupigana. Aidha mwandishi anaendeleza maudhui ya kuchapa kazi. Vijana wanashauriwa kufanya kazi badala ya kushiriki matendo ya kikaidi.

**3.5 Mazingaombwe ya mawazoni**

Kuna tukio la uhalisiamazingaombwe linalofanyika mawazoni mwa Champion.
Anawaona wasichana wa ajabu ambao haijulikani jinsi walivyofika hapo. Wasichana hawa wana uchu wa kufanya mapenzi wanapomwona Megido. Wanapomwita Megido anatoka mbio ili kwenda kushiriki mapenzi nao. Wasichana hao wanabadilika na kuwa wanyama.

Tukio la Champion kuwa mawazoni halafu awaone wasichana majitu wasiojulikana walikotoka ni la kushangaza. Wasichana hawa wanapojihusisha na kufanya mapenzi na Megido kisha wanageuka kuwa wanyama. Uhalisini mtu anapokuwa fikirani hana hata muda wa kulala kwa sababu anasumbuliwa na mawazo. Lakini hapa tunashuhudia Champion akiwa tu anatazama lakini anapoingia mawazoni ndipo kisa hicho cha ajabu kinapotokea. Mtunzi anatuarifu kupitia dondoo hili:

**Mfano (81)**

> "Megido!" Aliamshwa na Champion. Megido kwa upole aliamka. Champion alimuonyesha ishara ya mkono kuangalia upande wa pili. Megido aliona wasichana wawili mkabala wa chemchemi wakiwa kama walivyozaliwa-uchi, weupe, warembo na wenye nywele ndefu zilizolalia migongo yao. Wakiwa wanatazamana macho na wasichana wale, mara wale wasichana wakaanza kuwaita kwa ishara ya mkono. Megido alichanganyikiwa akiwa kasimama wima mwili wake ukionekana wenye uhitaji baada ya kukaa msituni kwa siku nyingi bila kuona utupu wa mwanamke…Megido alivutiwa na wasichana wale hata kusahau kila kitu na kutamani kwenda…Megido aliendelea kuelekea kwa wale wasichana nao wakamdaka na kuanza kufanya mapenzi, Kelele za mahaba zilisikika kwa nguvu hata zikageuka kuwa kelele za kutisha za wanyama wa ajabu.Mara pakasikika nyoka mbwa mwitu wa msitu mwenye kichwa tambarare…na mara hiyohiyo pakatokea nyoka tupa mwenye kichwa kipana chenye umbo la pembe tatu…sasa ilikuwa patashika kubwa kati ya nyoka hawa wawili. Kila nyoka akitaka kumwondoa uhai mwenzake. Mapigano haya yalitokea akilini mwa Champion. Alishuhudia mapigano hayo kwanzia mwanzo hadi mwisho."(uk 63-64)

Tukio hili la Champion kuwa mawazoni halafu amwone Megido akishiriki mapenzi na wale wasichana wanyama ni la uhalisiamazingaombwe. Ikumbukwe kuwa ndoto ni kipengele muhimu katika kazi za uhalisiamazingaombwe. Wamitila (2003) anasema kuwa katika nadharia ya uhalisiajabu ndoto huchukua nafasi muhimu sana. Matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Tukio la Megido kufanya mapenzi na wale wasichana wanaoonekana kama vitu ni tukio la kiuhalisiamazingaombwe ambalo ni nadra sana kufanyika katika maisha yetu ya kawaida. Uhalisini Ulrich Fusako hangeruhusu tendo kama lile kufanyika bali angezua vita. Mwandishi anaendeleza maudhui ya ukahaba. Ukahaba umekita mizizi katika mataifa mengi ya ulimwengu. Wanaume kwa wanawake sio waaminifu katika ndoa zao. Wamejiingiza katika ukahaba ili kukidhi haja za miili yao.

**3.6 Mazingaombwe ya kudaka risasi**

Kile kitendo cha Siprosa mkewe Megido kujitokeza katikati ya upepo ni cha uhalisiamazigaombwe. Riwayani tunashuhudia Inspekta Kadara akifyatua risasi ambayo Siprosa anaidaka kwa meno yake na kuitema chini. Matendo haya hayawezekani katika uhalisia. Hatujaelezwa jinsi alivyofika pale. Hata kule kudaka risasi iliyofyatuliwa na inspekta Kadara ni tendo la mazingaombwe kwani uhalisini risasi huua lakini kitendo tunachokishuhudia hapa kinatushangaza kwani baada ya kuidaka risasi na kuitema chini anapigana na Inspekta Kadara. Tunaarifiwa kupitia dondoo hili:

**Mfano (88)**

> "Kufumba na kufumbua, alimwona Siprosa mkewe Megido mbele yake akijitokeza katikati ya upepo ule. Alifyatua risasi ya kwanza. Siprosa aliidaka kwa meno yake na kuitema chini. *Bullet catch*. Kisha aliruka kumshambulia inspekta Kadara…" (uk 128).

Mwandishi ametumia tendo hili kuendeleza maudhui ya ulipizaji kisasi unaofanywa na tabaka la chini baada ya utawala ulio mamlakani kushindwa kuwatetea wanyonge kutoka mikononi mwa viongozi katili. Katika mataifa mengi, polisi wanaposhindwa kuwatetea wanyonge kutokana na nguvu za wanasiasa. Wanyonge huamua kupinga viongozi hawa na kukataa kabisa kudhulumiwa.

**3.7 Mazingaombwe ya hospitalini**

Tukio jingine la uhalisiamazingaombwe linafanyika hospitalini wakati wagonjwa wanapofungwa kwenye vitanda kwa mikanda, kuna wale waliokuwa wakirandaranda, mwingine alikuwa mielekani na mmoja wa walinzi pale. Dakika arobaini baadaye wagonjwa wengi wanaonekana wakiwa wamefungiwavitandani. Kuna maiti wanaoonekana wakiuma na kurandaranda hospitalini. Vurumai inajaa pale hospitalini kati ya wagonjwa na wafanyikazi. Manesi na wafanyakazi wengine wanatoroka.

Tukio hili ni la ajabu kwani uhalisini vurumai na fujo haijawahi kushuhudiwa hospitalini kwa sababu mgonjwa ni mtu aliye dhaifu na hawezi kupigana wala kufanya fujo kwa kukosa nguvu. Isitoshe maiti ni mtu aliyepoteza uhai na hisia na huhifadhiwa makafani akisubiri maziko. Maiti tunaokutana nao riwayani wanaonekana wakirandaranda na kuuma watu hospitalini. Tukio hili linaibua hofu kwa wasomaji wa riwaya hii japo tuna ufahamu kuwa lazima kuwepo na matukio ya kimiujiza katika kazi za uhalisiamazingaombwe ili kumfikirisha msomaji. Mtunzi anasema kupitia dondoo hili:

**Mfano (91)**

> "Dakika arobaini baadaye, wengi wa wagonjwa walikuwa wamefungiwa kwa njia moja au nyingine lakini kulikuwa na maiti chache zilizokuwa zinauma na kurandaranda hospitalini. Mmojawapo wa walinzi wa pale alishambuliwa. Kulikuwa na mkoromo na mgurumo na shingo la mlinzi yule ulipasuliwa na kuachwa wazi huku makelele yakijaa ukumbi wote. Manesi na wafanyakazi wengine ilikuwa ni mguu niponye. Kawaida ya kuta tulivu za hospitali pale Alepo ilikuwa ni ghasia-tupu. Wagonjwa walikuwa wanaendelea kufariki lakini sasa walikuwa wananguruma na kupiga kite na wakati huohuo walikuwa wanajirusha na kupigana na vitu walivyofungiwa." (uk 200-201).

Matukio yanayofanyika hospitalini yametumiwa kijazanda kueleza yale yanayofanyika katika mataifa mengi kati ya wafanyakazi na viongozi. Wagonjwa hapa wanatumika kuonyesha wafanyakazi wanyonge ilhali nesi Gracegor na kundi lake wanawakilisha viongozi serikalini ambao huwadhulumu wafanyakazi. Katika mataifa mengi barani Afrika kumeshuhudiwa migomo ya wafanyakazi inayotokana na kudhalilishwa kwao na viongozi. Wafanyakazi hulipwa mishahara duni ikilinganishwa na kazi wanazofanya. Mazingira wanamofanyia kazi huwa ni duni ndiposa tunawaona wagonjwa pale hospitalini wakipigana japo wamefungwa kwa mikanda. Wanapojaribu kulalamikia hali duni za kazi, wao hupuuzwa na viongozi na kutakiwa wanyamaze. Wafanyakazi hawa huamua kudai haki zao kwa njia ya fujo na ghasia ili waweze kusikilizwa.

**3.8 Mazingaombwe ya maiti kufufuka**

Maiti ni viumbe waliokufa na hawana uwezo wowote wa kuona wala kutenda Jambo lolote. Wale tunaokutana nao riwayani ni wa uhalisiamazingaombwe. Kuna wale wanaotenda matukio ya ajabu ambayo hayawezi kutendeka uhalisini. Baada ya kufa wanafufuka na kuanza kurandaranda katika mji wa Alepo. Polisi wanapowaua hawafi. Wanasikika wakigonga milango na kutoa sauti za ajabu.

Mtunzi anasema:

**Mfano (95)**

> "Katika orofa ya tatu, kikosi kile kiliwaangusha vizuu zaidi vilivyokuwa vimetapakaa pale… kile kikosi kilipata milango mingi iliyokuwa imefungwa huku mtu, ama kitu kikigonga mfululizo kwa ndani. Pa, pa, pa, sauti ilihinikiza na kutoa mwangwi kwenye kuta zilizokuwa wazi. Vile vitu vikijiangusha kwa mlango. Upande wa mwisho wa ukumbi ule, walimpata

mlinzi amelala kichalichali juu ya damu, vipande vya nyama vya mwili vikiwa vimenyofolewa kutoka uso wake na kichwa chake. Macho ya ile maiti yalifunguka!" (uk 217).

Tukio la maiti kufa na kisha kufufuka na kuanza kufanya vurugu kunaendeleza maudhui ya kutibuliwa kwa maandamano ya wafanyakazi wanapodai haki zao. Licha ya hayo yote, wafanyakazi huendelea kudai haki zao kutoka kwa walio mamlakani.

**IV: HITIMISHO**

Makala haya yamechunguza matumizi ya uhalisiamazingaombwe katika riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Mashetani wa Alepo*.Imedhihirika kuwa waandishi Said Ahmed Mohamed na Olali Tom wameathiriwa sana na suala la miujiza, Wamezungumzia kwa mapana sana matukio ya mazingaombwe yanayotendwa na wahusika wafu ambayo kwayo yanavuta hisia za woga kwa msomaji ilhali unapoyachunguza kwa kina yamebeba maudhui mazito katika jamii tunamoishi. Maudhui yanayojitokeza katika riwaya hizi yanamtaka msomaji kujirekebisha.

**MAREJELEO**


1. Cooper, B.(1995), *Magic Realism in West African Literature*, London; Routledge PublishingCompany.
2. Danow, K,D.(1995). *The spirit of The Carnival*.Magical Realism and the Grotesque. Kentucky. University Press of Kentucky.
3. Green, M. (2009). *Dreams of Freedom*. Magical Realism and Visionary materials in Okri and Blake, Romanticism 15/1-84
4. Khamis, S.A.(2007). Vionjo vya Riwaya Mpya katika Kioo cha Lugha,5,Tuki, Dar es Salaam. Mbatia, M. (1998). *"Mienendo katika uandishi wa Kezilahabi, Nagona na Mzingile,"* Mulika. Tol,24 (uk1-11).
5. Mkufya, W.E. (1999). *Ziraili na Zirani*. Dar es Salaam. Hekima Publishers.
6. Mohamed. S.A.(2013). *Mhanga Nafsi Yangu*.Nairobi. Standard Textbooks.
7. Njogu K, na Chimera, R.(1999) *Ufundishaji wa Fasihi katika shule*, Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation,
8. Njogu, K. na Wafula, R.M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
9. Olali, T. (2016). *Mashetani wa Alepo*; Nairobi.Jomo Kenyatta Foundation. Roh,F. (1925). *Magical Realism*: Durham; Duke University Press.
10. Senkoro, F.E.M.(2006). *Fasihi ya Kiswahili Simulizi na Fasihi Andishi katika kioo cha Lugha*,Juzuu ya 4, Tuki, Dar es Salaam.(Haijachapishwa)
11. Stretcher, M. (1999). *"Magical Realism and the search for identity in Fiction of Murakami."*Journal of Japanese studies. Juzuu, 25/2.
12. Wamitila, K.W.(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi. Vide- Muwa Publishers Limited.